**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI,**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI,**
**SHULE YA SEKONDARI MOSHI.**

**S.L.P 3021,**
**MOSHI**
**19.11.2025**

**Namba za simu:**

1. Kaimu Mkuu wa shule: 0765358489
2. Makamu wa Mkuu wa shule: 0787514688,
3. Walimu wa idara ya malezi: 0788190798, 0676404757

Kwa Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.......................................................................................

wa S.L.P.................................................................................................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MOSHI KWA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026.**

**1.** (i) Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Moshi mwaka 2026.

(ii) Shule ya sekondari Moshi iko umbali wa km 4 kutoka stendi kuu ya mabasi ya Moshi mjini barabara ya kuelekea hospitali ya KCMC mkabala na chuo cha polisi Moshi. Usafiri wa kutoka stendi ya mabasi Moshi mjini unapatikana kwa kutumia bajaji za kwenda KCMC kwa nauli ya Tsh 700/=.

(iii) Masomo yataanza tarehe 13.01.2026 kwa hiyo mwanafunzi aripoti shuleni tarehe 11.01.2026

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**A. SARE ZA SHULE.**

(i) Sare ya shule hii ni suruali mbili (2) za rangi ya KAKI, mashati mawili (2) meupe ya tetron yenye mikono mifupi (aina ya Tomato) na tai ya KAKI yenye mistari meupe.

**TANBIHI: Suruali iwe na rinda moja kulia na jingine kushoto kwa mbele na dart nyuma. Iwe na upana wa inchi 14 na iwe na turn up. Suruali za mtumba na vibamba (modo) haziruhusiwi shuleni.**

(ii) Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (2) vinavyofunika miguu na visiwe na kisigino kirefu.

(iii) Soksi jozi mbili za rangi nyeusi.

(iv) Bukta na fulana rangi ya njano na raba nyeusi kwa ajili ya michezo.

(v) Sweta mbili (2) za rangi ya brown (ugoro iliyokolea) zenye shingo ya **V.**

(vi) Mwanafunzi mwenye **Ualbino** aje na kofia ya rangi ya Khaki na mashati mawili meupe aina ya tomato yenye mikono mirefu.



CamScanner

(vii) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.
(viii) Mwavuli mkubwa kwa ajili ya mvua.
(ix) Mabuti ya mvua (Rain Boots) rangi nyeusi.
(x) Nguo za ndani za kutosha (boxer na singland)

**B. NGUO ZA KUSHINDIA (SHAMBA DRESS)**

(i) Mashati mawili ya draft ndogondogo yenye rangi ya blue yenye mikono mifupi.
(ii) Kwa wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi mashati yawe ya mikono mirefu.
(iii) Suruali mbili rangi ya blue masai
(iv) Track suit moja (1) rangi ya dark blue
(v) Viatu vya wazi (sandals) vya ngozi kwa ajili ya kuvaa jioni. **Yeboyebo haziruhusiwi**

**C. MAHITAJI YA TAALUMA**

(i) Plain paper (A4) bunda mbili (2) kwa mwaka kwa ajili ya majaribio na mtihani
(ii) Four Figure Mathematical tables (Form 1- 4)
(iii) Daftari 12 kubwa (counter books) na madaftari 12 aina ya msomi kwa ajili ya mazoezi.
(iv) Mathematical set, Kalamu za wino, Kalamu za risasi, rula n.k.
(v) Begi la mgongoni kwa ajili ya kubebea madaftari

**D. VIFAA VYA USAFI**

(i) Ufagio mmoja (1) wa chelewa mrefu
(ii) Dekio moja (1) aina ya pusher (rubber squizer)
(iii) sabuni ya maji aina ya Dexi (all purpose cleaner) aina nyingine ya sabuni haitapokelewa kabisa.

**E. MAHITAJI MENGINE**

(i) Godoro la sponji, urefu futi 6, upana futi 3 na unene inchi 4.
(ii) Shuka tatu (3) za rangi ya njano.
(iii) Blanketi moja (1).
(iv) Mto mmoja wa kulalia.
(v) Taulo, Mswaki, Dawa ya meno, Sabuni za kufulia na kuogea na malapa.
(vi) Chandarua cha Mbu
(vii) Vyombo vya kulia chakula kama bakuli, sahani, kikombe cha chai na kijiko
(viii) Ndoo ndogo mbili
(ix) Sanduku imara la bati (trunker) saizi ya kati na kufuli.
(x) Saa ya mkononi
(xi) Kopo la maji ya kunywa



CamScanner

**TANBIHI: (a) NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI SHULENI.**
**(b) NGUO ZOTE ZIWEKWE ALAMA KUEPUKA KUVALIANA NA KUIBIANA.**

**F: FEDHA ZA MATUMIZI MADOGO MADOGO (POCKET MONEY)**

Mzazi/Mlezi anaweza kumpa mwanaye fedha za matumizi binafsi. Fedha hizo zitatunzwa na ofisi ya malezi na mwanafunzi atapewa kidogo kidogo kupitia leja maalumu itakayofunguliwa kwa ajili ya kutunza kumbukumbu. Tunashauri mwanafunzi asipewe fedha nyingi ili kumwepusha na vishawishi na kuepuka kuibiwa.

**G : BIMA YA AFYA**

Mchango wa bima ya afya TSh (50,400/=) kwa wale wasio na kadi za bima ya afya (NHIF) uwekwe kwenye CRBD benki akaunti namba 0133691089900 OLD MOSHI SECONDARY. Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye *pay in slip* na aje nayo shuleni siku ya kuripoti. **Bima hii ni muhimu sana kwa kila mwanafunzi kuwa nayo.**

**FOMU ZILIZOAMBATISHWA**

(a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali ikiwa inaonesha hali halisi ya afya ya mwanafunzi.
Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara mwanafunzi atakaporipoti shuleni

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya Mzazi na Mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Pamoja na kukamilisha fomu zote hapo juu mwanafunzi anatakiwa kuja na:

i. Picha nne 4 (Passport size) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu picha hizi zibandikwe fomu D
ii. Aje na kivuli cha cheti cha kuzaliwa.
iii. Picha mbili (2) passport size za mwanafunzi. (awe amevaa shati la shule).

**VIPINDI VYA DINI.**

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuhudhuria vipindi vya DINI yake husika awapo shuleni.

Mwanafunzi anashauriwa kuja na vitabu au machapisho mbalimbali kwa ajili ya sala na vipindi vya dini kulingana na dini yake.



CamScanner

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Night Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni



CamScanner

**pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**KARIBU SANA MOSHI SEKONDARI**

**MARTIN P LINJE**

**KAIMU MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Kaimu Mkuu wa shule, 0765358489**
- **Makamu Mkuu wa Shule, 0787 514688**
- **Mwandamizi Taaluma 0754049940**
- **Mwandamizi Malezi 0788 190798**



CamScanner

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI**
**SHULE YA SEKONDARI MOSHI**

**FOMU A**

**HATI YA MAKUBALIANO**

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI MOSHI,
S. L. P 3021,
MOSHI

**KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE**

Mimi ............................................................................. nakubali nafasi ya kidato cha .................niliyopewa katika shule yako.

Ninayakubali masharti na kuwa nitatii sheria za shule hizo zilizoko na zile zitakazotolewa kwa muda wote wa masomo yangu. Naahidi kuwa nitawaheshimu na kuwatii walimu wote wa shule na wafanyakazi kama walezi wangu

Naahidi kuwa nitatii wale wote watakaoteuliwa au kuchagukliwa kuwa viongozi wangu kwa mujibu wa sheria

Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mwaminifu. Naahidi pia kuwa nitajielimisha kwa nguvu zangu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu.

Natambua kuwa nikikiuka ahadi hizi nitapoteza nafasi yangu hapa shule.

JINA LA MWANAFUNZI ..................................................SAHIHI ......................

JINA LA MZAZI/MLEZI ..................................................SAHIHI.......................

Anuani yaMzazi/Mlezi...........................................................................................

Simu namba/ .......................................................................................

Barua pepe (e-mail)..........................................................................................

Namba ya kuandikishwa ............................................. Tarehe............................

Darasa ulilopangiwa...........................Bweni...................... Block.......................

Jina la mwadili..........................................................................Sahihi..................



CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI**

**SHULE YA SEKONDARI MOSHI**

**FOMU B**

**MEDICAL FORM**

To be completed by medical officer from a recognized Government Hospital. Full Name of Student........................................Sex/Male.................. Blood count (Red and White) ............................................................

Stool examinations ......................................................................

Sexually Transmitted diseases.........................................................

T.B ................................................... Skin.............................. Eye test............................................Ears....................................

Chest.............................................Spleen....................................

Abdomen.......................................................................................

**ADDITIONAL INFORMATION**

E.g Physical defects/impairment /pediatric disorders.................................

I certify that the above is fit/unfit to pursue studies as stated above.

Signature ...................................................................................

**MEDICAL OFFICER**

DATE..................................Rubber Stamp...................................................

NOTE : Student should send or bring the completed form to school together.



CamScanner

CamScanner